

Maelezo Kuhusu Malariya kwa Wasafiri

Malariya ni nini?


malariya ni ugonjwa wewe unaweza kupata kutokana na kuumwa na mbu. Hakuna chanjo ambayo inaweza kukukinga na malariya.



malariya inaweza kuwa hatari sana. Njia bora za kuzuia malariya ni kuepuka kuumwa na mbu na kutumia dawa ulizoandikiwa na daktari unaposafiri na baada ya kurudi. Watu wanaweza kufa ndani ya muda wa saa 12 tangu kujisikia wagonjwa, hata kama wamewahi kuugua malariya awali.

Malariya huwa tatizo wapi?

Malariya ipo katika nchi nyingi. Nchi ambazo zimeoneshwa na rangi nyekundu na manjano ni mahali ambapo unaweza kuwa katika hatari ya kupata malariya.



Nani anaweza kupata malariya akiwa safarini?



Wasafiri wote—watoto NA watu wazima—wanaoenda nchi ambako kuna malariya wanapaswa kutumia dawa walizoandikiwa na daktari na kujaribu kuepuka kuumwa na mbu wakiwa katika safari yako.

HAUKO SALAMA kutokana na malariya hata kama umekuwa nayo mara nyingi awali.

Watu wanaweza kuwa na kinga fulani dhidi ya malariya ikiwa walishawahi kuwa nayo

mara nyingi awali, lakini kinga hiyo huisha, kawaida ndani ya miezi michache baada ya kuondoka kwenye eneo ambapo kuna malariya. Kutumia dawa za malariya na kuepuka kuumwa na mbu ndiyo njia bora ya kuhakikishwa kuwa wewe na familia yako mko salama.

Malariya inaweza kuwapatia watoto ugonjwa mkali, hasa watoto ambao wamekuwa wakiishi Marekani pekee. Watoto au watu wazima ambao hawajawahi kupata malariya wanaweza kufa haraka wanapopata ugonjwa huu.

Na itakuwaje nina ujauzito?

Kupata malariya ukiwa mjamzito kunaweza kukuhatarisha wewe na mtoto wako. Ni vyema kuepuka kusafiri kwenda sehemu zenye malariya wakati wa ujauzito.

Ukilazimika kusafiri, kuna dawa za malariya ambazo ni salama kumeza wakati wa ujauzito. Daktari wako atakusaidia kuchagua dawa ambayo ni nzuri zaidi kwako.



Dalili za malariya ni gani? Ninapaswa kufanya nini ikiwa ninazo?



Dalili za malariya ni pamoja na homa, kutetemeka, baridi, kuumwa na kichwa, maumivu ya misuli na kuchoka. Unaweza kusikia kama una mafua Unaweza pia kuwa unasikia kutapika, unatapika au kuhara. Malariya inaweza kuwa hatari ikiwa haitatibiwa haraka. Msafiri yeyote ambaye anapata ugonjwa wa homa au ugonjwa ambao una dalili kama za mafua anapaswa kwenda kumwona daktari. Unaweza kupata ugonjwa wa malariya ukiwa safarini au baada ya kurudi Marekani. Mwambie daktari wako kwamba ulikuwa katika nchi yenye malariya na ungependa kupimwa malariya.



Ili upate taarifa zaidi kuhusu malariya, tembelea www.cdc.gov na utafute 'malariya.'

Ili ujue kama malariya ni hatari katika maeneo unayosafiri, tembelea www.headinghomehealthy.com